

GRADE 2 MID TERM 3 DECEMBER 2021

4. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (Alama 5)

Sikiliza hadithi nitakayokusomea kisha nitakuuliza maswali.

Siku ya Jumatatu mawingu yalikuwa yametanda angani. Mwalimu wetu alituruhusu tuende nyumbani kabla ya mvua kunyesha. Kabla hatujafika nyumbani mvua ilinyesha ya mafuriko. Nyumba, miti na mifugo wengi walibebwa na mafuriko. Watu wengi walipata hasara sana.

- a) Mvua ilinyesha siku gani? (**alama 1**)
- b) Ni nani alituruhusu tuende nyumbani? (**alama 1**)
- c) Mvua ilinyesha ya aina gani? (**alama 1**)
- d) Mvua ilileta hasara gani? (**alama 2**)

5. KUSOMA KWA SAUTI

Soma hadithi hii kwa sauti.

Kila mmoja wetu ametoka kwa familia. Familia ina watu wengi. Kuna familia ambazo huwa na mzazi mmoja na familia nyingine huwa na wazazi wote wawili. Familia yangu ina mama, baba na watoto. Kwetu tuko watoto wanne. Kuna dada wawili na kaka wawili. Baba yetu hutufunza maadili na jinsi ya kuishi na watu wengine. Mimi ninaipenda familia yangu sana.

Mwanafunzi asome maneno 40 kwa dakika moja.